# Watu milioni 600 huathiriwa na chakula kisicho salama

NA FAUZIA MUSSA

ZAIDI ya watu milioni 600 huugua na 420,000 hufariki duniani kila mwaka kutokana na kula chakula kisicho salama ambapo asilimia 30 ya vifo hivyo vinahusisha watoto walio na umri chini ya miaka mitano.

Mtaalamu wa lishe kutoka Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Stella Kimambo, alieleza hayo katika maadhimisho ya Siku ya Usalama wa Chakula Duniani yaliyofanyika kwenye hoteli ya Golden Tulip, Zanzibar.

Alieleza kuwa takwimu za kimataifa zinathibitisha kuwa mamilioni ya watu huathiriwa kila mwaka kutokana na magonjwa yanayosababishwa na ulaji wa chakula kisicho salama jambo linalohitaji ushirikiano wa karibu baina ya serikali, sekta binafsi na jamii.

Aidha Kimambo alieleza kuwa pamoja na juhudi zinazoendelea duniani kote, magonjwa yanayotokana na chakula bado ni changamoto kubwa ya kiafya, hasa katika jamii masikini na kusema kuwa FAO itaendelea kushirikiana na serikali katika kuboresha maabara, kutoa elimu kwa wananchi na kuimarisha mifumo ya usalama wa chakula.

Katika kuongeza nguvu ya kukabiliana na hali hiyo alisisitiza umuhimu wa kuwekeza katika mifumo bora ya uzalishaji, usindikaji na uhifadhi wa chakula ili kupunguza athari za kiafya zinazotokana na kula chakula kisicho salama.

"Tunahitaji mifumo bora zaidi ya uzalishaji, usindikaji na uhifadhi wa chakula ili kupunguza madhara ya kiafya kwa walaji", alieleza Kimambo.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya ushauri, Wakala wa Chakula na Dawa (ZFDA), Dk. Salum Seif Salum, aliwataka wadau wote kushirikiana kikamilifu katika kutekeleza mkakati wa kitaifa wa usalama wa chakula na kusisitiza kuwa usalama wa chakula si suala la taasisi moja bali ni jukumu la pamoja.

Dk. Salum alieleza kuwa ni muhimu kila mmoja kuchukua hatua stahiki kwa nafasi yake katika kuhakikisha jamii inalindwa dhidi ya hatari zitokanazo na chakula na kusisitiza kuwa elimu zaidi inahitajika kwa wananchi hasa maeneo ya vijijini ambapo uelewa bado mdogo.

.

"Baadhi ya wajasiriamali wanauza chakula holela mtaani na kuwa na uhifadhi mbaya masokoni, jambo hili linahatarisha afya za walaji na kurudisha nyuma juhudi za serikali katika kuboresha usalama wa chakula", alisema Dk. Salum.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Udhibiti Usalama wa Chakula Zanzibar, Khadija Ali Sheha, alieleza hatua mbali mbali zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuhakikisha chakula kinachofika kwa mlaji ni salama.

Aliefafanua kuwa Zanzibar imepiga hatua kubwa katika uanzishaji wa maabara za kisasa na utoaji wa mafunzo kwa watendaji wa afya na wakaguzi wa chakula, lakini bado kuna haja ya kuongeza uelewa kwa umma kuhusu umuhimu wa usalama wa chakula kuanzia uzalishaji hadi mlaji.

"Tutaendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika masoko, migahawa na mahoteli sambamba na kutoa elimu kwa jamii juu ya njia sahihi za uhifadhi wa bidhaa za chakula ili kulinda afya ya mtumiaji", alisema.

Alibainisha kuwa ZFDA haiatasita kuziondoa sokoni bidhaa zilizokua si salama na kuitaka jamii kuendelea kushirikiana na wakala hao pindi wanapobaini uhifadhi usiosalama wa chakula ili kuongeza nguvu ya kumlinda mtumiaji.

Siku ya Usalama wa Chakula Duniani huadhimishwa kila mwaka ifikapo Juni 7 kwa lengo la kuhamasisha hatua za kuzuia, kugundua na kudhibiti hatari za kiafya zinazotokana na chakula ambapo siku hiyo mwaka huuimebeba kauli mbiu ya 'Usalama wa Chakula: Sayansi kwa vitendo'.



*MKURUGENZI Sera na Utafiti katika Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Ilyasa Pakacha Haji, akipanda miti katika eneo la Hifadhi ya Misitu Masingini ikiwa ni shamra shamra ya maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani. (PICHA NA WKUMM).*

# Miti 1,500 yapandwa Masingini kuadhimisha siku ya mazingira

NA SALAMA MOHAMMED, WKUMM

MITI 1,500 imepandwa katika hifadhi ya msitu wa Masingini, wilaya ya Magharibi 'A' Unguja katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani inayofikia kilele chake leo.

Zoezi hilo lililoratibiwa na Idara ya Misitu ya Wizara yaKilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo lilihusisha wadau mbali mbali ikiwemo Idara ya Mazingira katika Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ambapo Mkurugenzi Sera na Utafiti, ofisi hiyo, Ilyasa Pakacha Haji, alikuwa mgeni rasmi.

Akizungumza wakati wa zoezi hilo, Ilyasa alisema wameamua kuanza na upandaji wa miti na kufanyika shughuli za usafi ili kuhifadhi mazingira sambamba na kuihamasisha jamii juu ya matumizi sahihi ya nishati ya kupikia kupunguza matumizi ya ya kuni na mkaa.

Aidha Iliyasa aliwasisitiza wananchi wanaoishi kuzunguka msitu huo kuacha uharibifu wa misitu kwa matumizi binafsi ya ukataji miti na kuokota kuni.

Ilyasa pia aliwashauri wananchi hao kupanda miti isiyopungua mitatu na kuhakikisha wanaitunza, kuilinda na kuihifadhi kwa kua ni rasilimali muhimu kwa taifa.

"Ni vyema jamii ikahamasika kupanda miti ili kujikinga na maradhi yanayoweza kujitokeza sambamba na kutengeneza mazingira wezeshi ya vizazi vya sasa na baadae", alisema Iliyasa.

Alifafanua kuwa misitu ina msaada mkubwa kwa mazingira na viumbe hai hivyo jamii inapaswa kuilinda badala ya kuiharibu ili vizazi vya sasa na vya baadae viendelee kunufaika nayo kwa kuendeleza shughuli za kuihifadhi kwa maslahi yao na nchi kwa ujumla.

Kaimu Mkurugenzi Idara ya Misitu, Abass Juma Mzee, alisema wameamua kupanda miti pembezoni mwa baarabara ya msitu huo kutokana na ujenzi uliofanyika kuondoa baadhi ya miti na kuharibifu mazingira ya maeneo hayo.

"Ujenzi barabara ya Masingini - Kidichi inayokatiza kwenye eneo la hifadhi uliondoa baadhi ya miti hivyo tumeona umuhimu wa kuirejesha ili maeneo yaliyoharibiwa yawe katika hali yake baada ya ujenzi huo kukamilika", alieleza Abass.

Alieleza kuwa hatua hiyo mbali ya kuongeza haiba ya msitu huo, miti hiyo itaimarisha barabara na kupongeza ushirikiano walioupata kutoka Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais katika zoezi hilo.

"Siku ya Mazingira Duniani inasherehekewa katika kuona kwamba mazingira ya dunia yanaimarika kwa faida ya sasa na vizazi vijavyo sambamba na kurudisha ukijani katika visiwa vya Zanzibar", alisema Abass.

Aidha aliwapongeza wananchi wanaoishi pembezoni mwa msitu huo kwa kutunza mazingira na kupunguza uharibifu wa miti jambo linaloleta faida kwa vizazi vya sasa na baadae.

Mapema Mkuu wa Kikosi cha Utalii na Diplomasia, Kepteni Juma Saleh, alisema ushiriki wao katika zoezi hilo unatokana na umuhimu wa upandaji miti kwenye msitu wa Masingini ambao ni moja ya vivutio muhimu vya utalii nchini.

Alieleza kuwa idadi ya watalii imekuwa ikiongezeka Zanzibar hivyo Kamisheni ya utalii kwa kushirikiana na wadau wengine imeona haja ya kushiriki zoezi hilo ili kujionea vitu vingi kuhusu msitu huo maarufu nchini.

"Kama ulivyo msitu wa Jozani, msitu wa Masingini una vivutio vingi ambavyo vimetushawishi kuutumia kwa ajili ya kuwapeleka watalii kwa wingi kutokana na vivutio vingi vilivyopo katika msitu huo", alisema Kepteni Saleh.

# Kituo cha kilowati 570 za umeme jua chazinduliwa AOTTL

NA MWANDISHI WETU, Morogoro

KAMPUNI ya Puma Energy Tanzania imezinduzi rasmi wa kituo cha umeme wa jua chenye uwezo wa kilowati 570 katika kiwanda cha tumbaku cha Alliance One Tanzania Tobacco Limited (AOTTL).

Mradi huu uliopo Kinguluwira, Morogoro, takribani kilomita 200 kutoka jijini Dar es Salaam unatajwa kuwa ni hatua muhimu katika dhamira ya Puma Energy ya kuziwezesha sekta za viwanda Tanzania kwa suluhisho la nishati safi, nafuu na ya kuaminika.

Taarifa iliyotolewa jana na kampuni hiyo ilieleza kuwa kituo hicho kinajumuisha paneli 1,296 za solana 'inverter' 6 zenye ufanisi wa hali ya juu.

"Mfumo huu ulioounganishwa na gridi ya taifa umetengenezwa kutoa umeme wa kutosha wakati wa mchana kipindi chote cha uzalishaji wa kiwanda kuanzia Mei hadi Oktoba", ilieleza taarifa hiyo iliyomnukuu Mkurugenzi Mtendaji wa Puma Energy Tanzania, Fatma Abdallah.

Aliongeza kuwa mradi huo ni matokeo ya Mkataba wa Ununuzi wa Umeme (PPA) wa miaka 10 ulioingiwa kati ya Puma Energy na AOTTL mnamo mwezi Aprili 2024 ambao unahakikisha upatikanaji wa umeme safi na wa kuaminika huku ukipunguza kwa kiasi kikubwa utegemezi wa vyanzo vya kawaida vya umeme.

Ilielezwa kwamba ujenzi wa kituo hicho ulianza mwezi Machi 2025 na kukamilika mwezi Aprili, huku mfumo ukianza kufanya kazi rasmi kazi Mei 4, mwaka huu.

"Mradi huu wa sola katika kiwanda cha Alliance One ni mafanikio makubwa, si tu kwa Puma Energy bali pia kwa sekta ya viwanda Tanzania. Unadhihirisha dhamira yetu ya dhati ya kutoa suluhisho la nishati safi, nafuu na ya kuaminika linalowezesha biashara kustawi huku tukichangia katika ulinzi wa mazingira na mustakabali wa taifa letu", alisema Fatma.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa; "Tunajivunia kuwa mstari wa mbele katika mabadiliko haya ya nishati, tukionesha namna ubunifu unavyoweza kuchochea maendeleo ya kiuchumi sambamba na uwajibikaji wa kimazingira".

Aliongeza kuwa dhamana ya utendaji wa miaka 30, mfumo huu wa sola unahakikisha ufanisi wa nishati wa muda mrefu na uendelevu wa mazingira ikiwa ni ushahidi wa maono ya Puma Energy ya kuwezesha sekta ya viwanda Tanzania kupitia nishati safi, bunifu, na imara ili ya kukuza uchumi unaokwenda sambamba na utunzaji wa mazingira.